LIC LOCAL INVESTMENT CLIMATE

Brief No. 11

MRADI WA UFUGAJI SAMAKI (KIGOMA)

Mradi wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji (LIC) ni mradi wa kuendeleza sekta binafsi unaofadhiliwa na Danida. Mradi unashughulikia vikwazo vikuu vinavyokwamisha maendeleo ya biashara na ukuaji wa uchumi katika ngazi ya wilaya kwenye mikoa miwili ya Dodoma na Kigoma nchini Tanzania. LIC imejikita katika mijadala kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, miundombinu ya utoaji wa huduma za biashara ikiwa ni pamoja na vituo vya pamoja vya biashara na miundombinu ya pamoja kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kusaidia maendeleo ya biashara na uwekezaji. Washirika wanaotekeleza mradi wa LIC ni Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Sekretariati za mikoa ya Kigoma na Dodoma, Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) Tanzania, Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA).

Ufugaji wa samaki umetambuliwa kuwa miongoni mwa fursa nzuri ya biashara ambayo haijatumiwa sana nchini Tanzania. Aina za samaki wanaoweza kuleta faida zinajumuisha samaki aina ya Sato na Hongwe/Kambare wanaozalishwa kwenye maji baridi na Mwani, Kaa, Koazi na Kamba wanaozalishwa kwenye maji chumvi. Hata hivyo sekta hii bado inakabiliwa na ukosefu/upungufu wa bembejeo zenye ubora za ufugaji wa samaki (vifaranga, mbegu na vyakula bora vya samaki) teknolojia hafifu, ujuzi mdogo na viwango vya chini vya uwekezaji.

Mnamo Oktoba 2018, mradi wa LIC kupitia programu yake ya vijana na biashara – ulifanyia kazi ombi la kundi la vijana la 'One Word Group' kuunga mkono utekelezaji wa mradi wa ufugaji wa samaki huko Kibirizi, mkoani Kigoma. Kundi la 'One Word Group' lina wahitimu waliomaliza masomo hivi karibuni kutoka Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) mkoani Kigoma na sasa linapokea msaada kutoka LIC ili kuzalisha samaki kwaajili ya matumizi ya ndani. Ili kutumia fursa ya uhitaji mkubwa uliopo kwa sasa, kundi hilo pia litazalisha samaki na vifaranga vya samaki kwa kwa ajili ya kuwauzia wafugaji wengine na wamiliki wa mabwawa ya samaki mkoani Kigoma na hatimaye kwenda mbali zaidi. Aidha, kundi hilo litatoa mafunzo na huduma za ugani kwa wafugaji wa samaki.

Mwaka 2017, kundi hilo liliweza kuanzisha bwawa moja la majaribio na kuweka vifaranga 1,000 vya samaki aina ya Sato. Mavuno ya kwanza yalifanyika mnamo Agosti 2018. Msaada wa LIC kwa kikundi ni pamoja na mita yenye kuangalia ubora wa maji, mashine ya kulishia yenye uwezo wa kuzalisha tani 0.12-0.15 kwa saa, mashine ya kusaga nafaka yenye uwezo wa kuzalisha tani 1.5 kwa siku, masanduku 10 ya Kuhifadhi baridi, mfumo wa nishati ya umeme jua, vifaa vya kuvunia, vifaa vya uzio na mabomba ya maji.

LIC imesaidia pia wanachama wa Kikundi cha One Word Group kushiriki katika mafunzo ya wiki moja ya kilimo biashara na mafunzo ya siku tatu katika shamba la samaki la Ruvu, mkoa wa Pwani. Yakiongozwa na mtaalamu wa uzalishaji wa samaki, ambaye amekuwa katika biashara kwa miaka 8, mafunzo kwenye shamba la samaki yalikuwa yenye manufaa sana. Wakiwa tayari kuanza biashara yao, kundi la One Word lilipata awamu ya kwanza ya vifaranga vya samaki Disemba 2018 kutoka Mbeya, na awamu ya pili kutoka shamba la samaki la Ruvu mwezi Januari 2019.

Mashine ya kutotolea mayai ya samaki

Bwawa la kufugia vifaranga vya samaki

Mambo Muhimu ya Mradi na Mafanikio

Kundi limejenga mabwawa matatu ya samaki – mabwawa mawili yana uwezo wa kuchukua vifaranga vya samaki 3,000 na la tatu lina uwezo wa kuchukua vifaranga vya samaki 5,000. Mabwawa hayo yalijazwa vifaranga vya samaki aina ya Sato. Mabwawa hayo mawili yanatarajiwa kuzalisha mavuno ya kwanza ifikapo Julai 2019 na samaki kutoka bwawa la tatu watavunwa ifikapo Oktoba 2019.

Bwawa la samaki

Mashine ya kuzalishia chakula cha samaki

Msaada huu wa mfano kutoka LIC kwa kundi la ufugaji wa samaki la One Word unatarajiwa kuchochea hamasa katika biashara ya ufugaji wa samaki baina ya wawekezaji wengine mkoani. Wawekezaji hawa wapya wanaweza kununua vifaranga na chakula cha samaki kutoka Kundi la One Word, pindi tu watakapoanza uzalishaji. Sehemu nyingi za mkoa wa Kigoma zimebarikiwa kuwa na maji ya kutosha na kilimo cha samaki kinaweza kuwa biashara muhimu kwa wazalishaji wengi wadogo na wa kati.

Zaidi ya hayo, inatarajiwa kwamba aina hii ya msaada wa LIC kwa makundi ya vijana wanaojihusisha na kilimo biashara utaigwa na mashirika mengine yanayosaidia vijana na vikundi vingine vya vijana. Huduma za ugani na mafunzo zinazotolewa na kundi la One Word litawawezesha wengine kufuata - sio tu katika ufugaji wa samaki lakini katika kuanzisha biashara ndogo ndogo kwa ujumla, kwa kutumia mkakati wa kuanzisha biashara wa kundi la One word. Kundi hili limeonyesha nia kubwa ya kujitoa na kufanya kazi kwa bidii kufikia malengo yao, ambayo daima yamekuwa kichocheo cha mafanikio katika biashara. Mfano huu halisi wa kikundi hiki cha vijana chenye kujitoa hakika utakuwa mfano wa nguvu na ukumbusho wa jinsi ya kufikia mafanikio kwa wengine kufuata.

LIC imewekeza takriban kiasi cha shilingi milioni 37 katika uanzishaji wa ufugaji wa samaki wa kundi la One Word. Mradi wa LIC ulianza tangu mwaka 2014 na utaendelea kusaidia miradi ya maendeleo ya sekta ya umma na sekta binafsi katika mikoa ya Kigoma na Dodoma mpaka mwaka 2020.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti ya mradi wa LIC: www.lic.or.tz

Februari 2019